

Dodoso la CRAFFT 2.1+N

Kujazwa na mgonjwa

Tafadhali jibu maswali yote kwa uaminifu; majibu yako yatawekwa kwa siri.

Kipindi cha MIEZI 12 ILIYOPITA, ni kwa siku ngapi:

- | | |
|---|--------------------------------|
| 1. Ulikunywa mafunda zaidi ya bia, mvinyo, au kinywaji chochote kilicho na pombe? Weka "0" ikiwa hamna. | <input type="text"/> Siku # |
| 2. Ulitumia marijuana (bangi, mafuta au nta kwa kuvuta, kufusha, kutona au katika vyakula) au " marijuana ya kusanisi " (kama "K2," "Spice")? Weka "0" ikiwa hamna. | <input type="text"/> Siku # |
| 3. Ulitumia kingine chochote kulewa (kama vile dawa haramu, dawa za maagizo na zisizo za maagizo na vitu unavyonusa, kupumua, kufusha, au kujidunga)? Weka "0" ikiwa hamna. | <input type="text"/> Siku # |
| 4. Ulitumia kifaa cha kufusha* kilicho na nikotini na/au ladha , au unatumia bidhaa zozote za tumbaku†? Weka "0" ikiwa hamna. <i>*Kama vile sigara za dijitali, modi, vifaa vya podi kama JUUL, mafusho ya kutupa kama vile Puff Bar, kalamu za mafusho, au e-hookahs. †Sigara, siga, cigarillos, hookahs, kutafuna tumbaku, ugoro, snus, au viyeyukaji.</i> | <input type="text"/> Siku # |

SOMA MAAGIZO HAYA KABLA YA KUENDELEA:

- Ukiweka "0" katika visanduku VYOTE hapo juu, JIBU SWALI LA TANO HAPA CHINI, KISHA UACHE.
- Ukiweka "1" au zaidi kwa Maswali ya 1, 2, au 3 hapo juu, JIBU MASWALI 5-10 HAPA CHINI.
- Ukiweka "1" au zaidi kwa Swali la 4 hapo juu, JIBU MASWALI YOTE YALIYO KWENYE UKURASA WA NYUMA.

Chorea mduara moja

- | | |
|---|----------------------------|
| 5. Umewahi kupanda GARI linaloendeshwa na mtu (ikiwemo wewe mwenyewe) aliyekuwa "mlevi" au alikuwa akinywa pombe au kutumia dawa za kulevya? | Hapana Ndiyo |
| 6. Je, unakunywa pombe au unatumia dawa za kulevya KUTULIA, kuhisi vizuri kujihusu, au kufaa? | Hapana Ndiyo |
| 7. Je, unakunywa pombe au unatumia dawa za kulevya ukiwa PEKE YAKO? | Hapana Ndiyo |
| 8. Je, UNASAHAU mambo uliyofanya unapokunywa pombe au kutumia dawa za kulevya? | Hapana Ndiyo |
| 9. Je, FAMILIA au MARAFIKI zako hukuambia kuwa unapaswa kupunguza kulewa au kutumia dawa za kulevya? | Hapana Ndiyo |
| 10. Je, umewahi kujipata MATATANI ukinywa pombe au ukitumia dawa za kulevya? | Hapana Ndiyo |

NOTISI KWA WAFANYAKAZI WA KLINIKI NA REKODI ZA MATIBABU:

Taarifa zilizo kwenye ukurasa huu zimelindwa na kanuni maalum za usiri za serikali kuu (42 CFR Sehemu ya 2), ambazo zinapiga marufuku ufichuaji wa taarifa hizi isipokuwa iwe imeidhinishwa kwa kibali maalum cha maandishi

Reproduced with permission from the Center for Adolescent Behavioral Health Research (CABHRe), Boston Children's Hospital.

For more information and versions in other languages, see www.crafft.org.

© John R. Knight, MD, Boston Children's Hospital, 2020.

Maswali yafuatayo yanauliza kuhusu matumizi yako ya **vifaa vyovyote vya kufusha vilivyo na nikotini na/au ladha**, au matumizi ya **bidhaa zozote za tumbaku***. Chorea mduara jibu lako kwa kila swali.

Chorea mduara moja

| | | | |
|----|---|--------------|---------------|
| 1. | Je, umewahi kujaribu kuacha kutumia, lakini ukashindwa? | Ndiyo | Hapana |
| 2. | Je, unafusha au unatumia tumbaku <u>sasa</u> kwa sababu ni vigumu sana kuacha? | Ndiyo | Hapana |
| 3. | Je, umewahi kuhisi kama uliye na uraibu wa kufusha au kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |
| 4. | Je, wewe huwa na hamu nzito ya kufusha au kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |
| 5. | Je, umewahi kuhisi kama uliyehitaji sana kufusha au kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |
| 6. | Je, ni vigumu kuacha kufusha au kutumia tumbaku katika maeneo ambapo hupaswi kufanya hivyo, kama shuleni? | Ndiyo | Hapana |
| 7. | Wakati hujafusha wala kutumia tumbaku kwa muda fulani (au wakati ulijaribu kuacha kutumia)... | | |
| a. | je, ulipata changamoto kumakinika kwa sababu ulishindwa kufusha au kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |
| b. | je, ulihisi kukereka zaidi kwa sababu usingeweza kufusha wala kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |
| c. | je, ulihisi haja au hamu nzito ya kufusha au kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |
| d. | je, ulihisi woga, kukosa utulivu, au wasiwasi kwa sababu usingeweza kufusha wala kutumia tumbaku? | Ndiyo | Hapana |

*Marejeo:

Wheeler, K. C., Fletcher, K. E., Wellman, R. J., na DiFranza, J. R. (2004). Kuwachunguza vijana kwa ajili ya kutegemea nikotini: Hooked On Nicotine Checklist. *J Adolesc Health*, 35(3), 225–230;

McKelvey, K., Baiocchi, M., na Halpern-Felsher, B. (2018). Matumizi na Dhana za Sigara za Dijitali Kulingana na Pod ya Vijana na Wazee Vijana. *JAMA Network Open*, 1(6), e183535.

NOTISI KWA WAFANYAKAZI WA KLINIKI NA REKODI ZA MATIBABU:

Taarifa zilizo kwenye ukurasa huu zimelindwa na kanuni maalum za usiri za serikali kuu (42 CFR Sehemu ya 2), ambazo zinapiga marufuku ufichuaji wa taarifa hizi isipokuwa iwe imeidhinishwa kwa kibali maalum cha maandishi

Reproduced with permission from the Center for Adolescent Behavioral Health Research (CABHRe), Boston Children's Hospital. For more information and versions in other languages, see www.crafft.org.

© John R. Knight, MD, Boston Children's Hospital, 2020.